**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

Mwenyekiti
Wajumbe Bodi ya Zabuni,

**Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe**

Idara: AFYA
CR No:-**06/2021/2022**
Tarehe: **14/01/2022**

**YAH: MAOMBI YA IDHINI YA KURIDHIA TAARIFA YA TATHMINI YA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARULA (EMD) NA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUMISHI (THREE IN ONE) KWA KUTUMIA NJIA YA ZABUNI**

Kifungu cha Kanuni Na 58(1) cha Tangazo la Serikali Na. 446 cha Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 mabadiliko yake ya mwaka 2016 yametoa mamlaka kwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni kufanya maamuzi bila kuweka kikao.

Itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 26/11/2022 Kitengo cha Manunuzi kiliwasilisha ajenda ya maombi idhini ya ujenzi jengo la Wagonjwa wa dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu na Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (Three in One) kwa kutumia njia ya zabuni ya wakandarasi.

Aidha, kufuatia maelekezo yaliyotolewa na OR TAMISEMI; Kitengo cha Manunuzi kilitangaza zabuni hiyo kupitia Mfumo wa Manunuzi wa TANePS ambapo baada ya ufunguzi kufanyika kila zabuni tajwa hapo juu matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

**a) Ujenzi jengo la Wagonjwa wa dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu**

| **S/N** | **Jina la Mzabuni** | **Kiasi (Tshs)** |
|---|---|---|
| 1 | KIUNGA BUILDERS (TANZANIA) LIMITED | 1,048,049,901.00 na VAT |

**Kazi ya uchambuzi zabuni**

Kazi ya uchambuzi wa zabuni imefanyika kwa njia ya mfumo wa TANePS katika hatua tatu yaani uchambuzi wa sifa za awali, uchambuzi wa kina na Uchambuzi wa sifa za ziada.



CamScanner

a) **Uchambuzi wa sifa za awali**

Katika uchambuzi wa sifa za awali, taarifa ya tathmini inaonesha kuwa kati ya wazabuni wawili walioomba zabuni hii mzabuni mmoja ambae ni M/s KIUNGA BUILDERS (TANZANIA) LIMITED ambaye alipita katika vigezo vya sifa za awali hivyo kuendelea katika hatua ya sifa za kina.

b) **Uchambuzi wa kina**

Kufuatia uchambuzi wa sifa za awali uliofanyika, timu ya tathmini ilipendekeza Mzabuni M/s KIUNGA BUILDERS (TANZANIA) LIMITED kuendelea kuchambuliwa katika uchambuzi wa kina kwa kuanza ukokotoaji wa Ankara za bei (BOQ) aliyowasilisha.

Katika vigezo tajwa hapo juu, taarifa inaonesha kuwa Timu ya Uchambuzi ilibaini kuwa pamoja na kuonekana kwenye ufunguzi gharama yake kuwa Tshs. 1,048,049,901.00 na VAT mara baada ya uchambuzi wa Ankara zake ilibainika kuwa gharama halisi zilizokokotolewa ni Tshs. 575,492,726.00 ingawa gharama yake ipo juu ya bajeti ya Mwajiri ya kiasi cha Tshs. 300,000,000.00 tu.

c) **Uchambuzi wa sifa za ziada**

Timu ya Uchambuzi ilifanya uchambuzi wa sifa za ziada za Mkandarasi. Taarifa inaonesha kuwa katika vigezo vyote vilivyotolewa Mkandarasi huyu katika uzoefu, watalaamu wake, mitambo, uwezo wa kifedha n.k

**Mapendekezo ya Timu ya Tathmini**

Timu ya Uchambuzi imeeleza kuwa kufuatia uchambuzi uliofanyika katika vigezo tajwa hapo juu, timu ya tathmini inapendekeza zabuni hii kufanywa na Mwekezaji M/s KIUNGA BUILDERS (TANZANIA) LIMITED, Dodma kwa masharti ya kufanya majadiliano katika kipengele cha gharama za mradi ya tshs. 575,492,726.00 kwa kulinganisha na bajeti iliyopo ya Tshs. 300,000,000.00.

Kufuatia taarifa hiyo, Kitengo cha Manunuzi kilipitia kwa kina taarifa hiyo na mapendekezo yake na kuridhia mapendekezo yaliyotolewa na timu ya tathmini. Hata hivyo; Halmashauri imepokea barua yenye kumb. Na. AH.161/298/01 ya tarehe 13/01/2022 ikiagiza kuwa utekelezaji wa miradi tajwa hapo juu kutumia njia ya "Force Account" kutokana na gharama kubwa zilizojazwa na wakandarasi karibu kwa Halmashauri zote nchini.

## b) Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (Three in One) katika Kituo cha Afya Kyimo

| S/N | Jina la Mzabuni | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | NESHAL INVESTMENT COMPANY LIMITED | 145,647,900.00 na VAT |

**Kazi ya uchambuzi zabuni**

Kazi ya uchambuzi wa zabuni imefanyika kwa njia ya mfumo wa TANePS katika hatua tatu yaani uchambuzi wa sifa za awali, uchambuzi wa kina na Uchambuzi wa sifa za ziada.

a) **Uchambuzi wa sifa za awali**
Katika uchambuzi wa sifa za awali, taarifa ya tathmini inaonesha kuwa kati ya wazabuni wawili walioomba zabuni hii mzabuni mmoja ambae ni M/s NESHAL INVESTMENT COMPANY LIMITED ambaye alipita katika vigezo vya sifa za awali hivyo kuendelea katika hatua ya sifa za kina

b) **Uchambuzi wa kina**
Kufuatia uchambuzi wa sifa za awali uliofanyika, timu ya tathmini ilipendekeza Mzabuni M/s NESHAL INVESTMENT COMPANY LIMITED kuendelea kuchambuliwa katika uchambuzi wa kina kwa kuanza ukokotoaji wa Ankara za bei (BOQ) aliyowasilisha.

Katika vigezo tajwa hapo juu, taarifa inaonesha kuwa Timu ya Uchambuzi ilibaini kuwa pamoja na kuonekana kwenye ufunguzi gharama yake kuwa Tshs. 145,647,900.00 na VAT mara baada ya uchambuzi wa Ankara zake ilibainika kuwa gharama halisi zilizokokotolewa ni Tshs. 145,647,900.00 ingawa gharama yake ipo juu ya bajeti ya Mwajiri ya kiasi cha Tshs. 90,000,000.00 tu.

c) **Uchambuzi wa sifa za ziada**
Timu ya Uchambuzi ilifanya uchambuzi wa sifa za ziada za Mkandarasi. Taarifa inaonesha kuwa katika vigezo vyote vilivyotolewa Mkandarasi huyu katika uzoefu, watalaamu wake, mitambo, uwezo wa kifedha n.k

**Mapendekezo ya Timu ya Tathmini**

Timu ya Uchambuzi imeeleza kuwa kufuatia uchambuzi uliofanyika katika vigezo tajwa hapo juu, timu ya tathmini inapendekeza zabuni hii kufanywa na Mwekezaji M/s NESHAL INVESTMENT COMPANY LIMITED, Mbeya kwa masharti ya kufanya majadiliano katika kipengele cha gharama za mradi ya tshs. 145,647,900.00 kwa kulinganisha na bajeti iliyopo ya Tshs. 90,000,000.00.

Kufuatia taarifa hiyo, Kitengo cha Manunuzi kilipitia kwa kina taarifa hiyo na mapendekezo yake na kuridhia mapendekezo yaliyotolewa na timu ya tathmini. Hata hivyo; Halmashauri imepokea barua yenye kumb. Na. AH.161/298/01 ya tarehe 13/01/2022 ikiagiza kuwa utekelezaji wa miradi tajwa hapo juu kutumia njia ya "Force Account" kutokana na gharama kubwa zilizojazwa na wakandarasi karibu kwa Halmashauri zote nchini.

Mwenyekiti na Wajumbe ninaomba kuwasilisha kwenu ajenda hii ikiwa ni pamoja taarifa ya uchambuzi wa zabuni hii kwa maamuzi zaidi ya kusitisha kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kutumia Wakandarasi na badala yake kutekeleza zabuni hii kwa njia ya manunuzi ya "Force Account" kama maelekezo ya OR TAMISEMI yalivyotolewa.



CamScanner

Naomba kuwasilisha.

...........................................

Victor A. Mwakapala

**KATIBU – BODI YA ZABUNI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

**MAAMUZI YA WAJUMBE WA BODI YA ZABUNI JUU YA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARULA (EMD) NA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUMISHI (THREE IN ONE) KWA KUTUMIA NJIA YA ZABUNI**

| NA. | JINA LA MJUMBE | MAONI YA MJUMBE | SAHIHI |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | Feliche T. Kigava | Naridhia | [signature] |
| 3. | Auckland Ihyesa | Naridhia | [signature] |
| 4. | PHILIPO A Mwakibete | Naridhia | [signature] |
| 5. | | | |

**IMETHIBITISHWA NA:-**

...........................................

Bw. Gerald Kifyasi

**MWENYEKITI**

**TAREHE**...14/01/2022...........

...........................................

Bw. Victor A. Mwakapala

**KATIBU**



CamScanner